

## NANI ANAWEZA KUNISAIDIA ?

### AHUKO PEKE YAKO; HUDUMA ZIFUATAZO ZINAWEZA KUKUSAIDIYA:

Ili **KUSIKILIZWA**, kupata **MAELEZO**,  
**MWONGOZO** (kupata malazi, huduma za  
kisheria, usaidizi wa kijamii au kisaikolojia, ...)

**0800 30 030** (masaa 24/24 kila siku, bila  
malipo na bila kujulikana) au **ongee** kwa  
ujumbe kwenye anuani  
[www.ecouteviolencesconjugales.be](http://www.ecouteviolencesconjugales.be)

**UKIWA HATARINI**. Pigia simu **polisi** kwa  
namba 101 au lombaa **msaada** kwa namba  
**112**

## MHAMIAJI NA MWATHIRIWA WA UJEURI KATIKA NDOA AU KATIKA FAMILIA



ULIKUJA UBELJII KUJIUNGA  
NA MEMBA WA FAMILIA ZAKO  
NA UNAISHI HALI YA UJEURI  
NYUMBANI?

Écoute Violences Conjugales  
**0800 30 030**  
24/7 + GRATUIT + ANONYME



Wallonie

Kipeperushi hiki kimebuniwa kutoka kwenye brosha ya «Mhamiaji na mwathiriwa wa Ujeuri wa nyumbani, ni zipi haki zangu», iliyotayarishwa na "CIRE" na jukwaa husiani la Brussels "ESPER".

## NI NINI UJEURI KATIKA NDOA AU FAMILIA ?

UJEURI KATIKA NDOA AU FAMILIA INAWEZA KUWA :

### UTAWALA

tishio ya kunyanganywa makaratasi vya Sheria, ao kukurudisha inchini yako



### KIFEDHA

kuacha mtu bila pesa, bila chakula, bila mashini ya kuleta joto



### KIMWILI

kupigwa, kusukumwa, Kumnyonga kwa kitazi



### UJINSIA

kulazimu au kulazimisha mwingiliano wa kingono kwa nguvu



### MANENO

kutukana, kutishia



### KISAIKOLOJIA

kutishia, kutia kizuizini, kuzuia mtu kusoma au ku fanya kazi, kufedhehesha na kudhalilisha



## WEWE NA WATOTO WAKO MNA MA HAKI

Mna haki ya **kuishi bila ujeuri**. Ujeuri ndani ya ndoa au katika familia ni hatia chini ya sheria za Ubeljiji.



Mna haki ya **kuongea na watu walio karibu na nyinyi ambao wanaweza kuwasaidia na kuwaongoza**: familia yako, daktari wako, OFISI ya Uzazi na Utoto (ONE), shule ya watoto...



Pia una haki ya **kuitisha usaidizi na kuripoti kwa polisi**.



Hata kama cheti chako cha ukaazi kinategemea wewe kuishi na mume wako, mke wako au familia yako, una haki ya **kutoka nyumbani**.



Ulizia na hifadhi ithibati ushahidi wa ujeuri : vyeti vya kimatibabu, ripoti za polisi, ushahidi, picha, baruapepe, SMS, rekodi...

Ili kudumisha **cheti chako cha ukaazi**, ni lazima ukidhi mahitaji fulani. Wakili au watoa huduma zilizofanywa maalum wanaweza kukusaidia.

